**Deni la Rashid Sultan**
Hakukuwa na jambo lolote la kipekee kuhusu kijiji ambacho Rashid Sultan na familia yake walikuwa wanaishi. Kadhalika hakukuwa na kitu cha kipekee kwa Rachid Sultan na familia yake. Alikuwa na duka dogo ambalo lilimpa faida ndogo ka ajili ya kumtunza yeye na familia yake, lakini haikutosha kuimarisha biashara yake.

Siku moja Rashid alisikia kutoka kwa rafiki yake kwamba kazi nzuri mahali fulani katika nchi jirani mbali kidogo na nchi yake ya asili. Kule alihakikishiwa kuwa atakuwa na kipatokizuri kwa ajili ya maisha yake ya baadaye.

Rashid alifurahia sana wazo hili, akaamua kwenda kujaribu bahati yake katika nchi ya ugeni. Aliuza duka lake na kutumia fedha alizopata kulipia gharama za usafiri na kuacha kiasi kidogo kwa familia yake (ambayo alitumaini itamfuata baadaye) na kubakiza kiasi kidogo cha kumsaidia atakapokuwa katika nchi ya ugenini.

Alipofika kule ugenini, alipata nyumba ya gharama nafuu, akalipa amana na kuanza kutafuta kazi. Lakini, chakusikitisha ni kwamba kutafuta kazi ilikuwa jambo gumu sana. Kila siku aliendelea kutafuta kazi na kila siku akiba yake iliendelea kupungua.
Bila kuwa na pesa ange-kulaje? Mara akagundua kuwa hana fedha za  kutosha hata kulipia kodi ya nyumba.

Baada ya miezi miwili, mwenye nyumba akaja kukusanya kodi. Ulikuwa wakati mgumu sana kwa Rashid. "Bwana," alisema, "tafadhali nivumilie. Sijapata kazi na hivyo siwezi kulipa kodi ya nyumba unayonidai”. Mwenye nyumba, mtu mpole, alimwangalia kwa jicho la huruma akakubali kuahirisha kukusanya kodi.

Rashid akaendelea kutafuta kazi, lakini ikashindikana. Katika mwezi wa tatu akagundua kwamba hakuwa na kitu ambacho angeweza kuongeza isipokuwa deni na wasiwasi. Mwenye nyumba akaja na kwa mara nyingine Rashid akapatwa na aibu.

Kwa maneno mabaya akaamua kuvunja ukimya wake: ‘’Bwana, watu wanasema kwamba wewe ni mtu mkarimu. Nisamehe deni la miezi mitatu iliyopita. Kuanzia sasa nitakulipa’’.
‘’Ni Kweli’’, mwenye nyumba alimjibu, "Mimi ni mtu mwenye huruma na mkarimu, lakini mimi ni mwanadamu pia. Ni lazima ulipe deni lako, kwa sababu malipo ya deni lako baadaye hayataweza kufunika deni lako la nyuma.

Niruhusu nikushauri kwamba usiruhusu madeni yako yaongezeke kiasi cha kukushinda”.
Baada yakusema maneno hayo mwenye nyumba akaondoka.

Muda ukapita. Mwisho wa mwezi wa Ramadhani, mwezi ule wa mfungo, Rashid hakuwa na kitu cjochote cha kufungulia isipokuwa mkate mkavu – bila ya kutaja deni lake kubwa lililokuwa likimsimamia kama mnyororo uliozunguka shingon yake.

Kwa hakika mwenye nyumba atarudi wakati wa Sikukuu kubwa, na sasa alikuwa akiogopa kuja kwa sikukuu hio. Kama hatalipa kodi yake, bila shaka atatolewa na kutupwa barabarani na kukosa mahali pa kuishi katika nchi ya ugenini.
Ikafika ile Siku kuu ya kuchinja na Rashid hakuwa na kondoo wa kuchinja wala nguo nzuri za kuvaa. Alipokuwa akienda nyumbani hadi nyumba kuomba, kila mmoja wao alikataa. "Ndugu, wewe na mimi tuko katika hali moja," kila mmoja alimjibu siwezi kukupa au

kukuazima kile ambacho sina. Maana hata mimi ni mdaiwa na ninasubiri tu kile kitakachonitokea”.

Ndipo Rashid alipoamua kuachana na juhudi zake za kutaka kukopa fedha. Siku iliyofuata alifunga, akainamisha kichwa chake katikati ya magoti yake akifikiria hatua nyingine atakayoichukua. Hali hii ya kukata tamaa iligeuka na kumfanya kuwa na hasira na chuki. Mara, kama Rachid alivyokuwa akitazamia akaskia mtu akigonga mlangoni wakati ule wa usiku. Hakuwa mwenye nyumba, bali mtoto wa mwenye nyumba. Rachid akiwa na hasira, alimwambia yule
mtoto wa mwenye nyumba kwamba asingependa kumuona. Pamoja na mapokezi mabaya ambayo Rashid alimwonyesha, yule mtoto wa mwenye nyumba alimnyooshea mkono wa upendo na urafiki na kusema naye kwa upole kwa maneno ambayo yalituliza moyo wake na hasira:

“Ndugu yangu, sikuja kukukaripia lakini kukuletea habari njema. Baba yangu na mimi tumeuona umasikini wako na tuna huruma kwa ajili yako. Na tunajua pia kwamba uma huzuni kuu zaidi kwa sababu hapa uko mbali na nyumbani. Ni kweli kwamba baba yangu ni mtu wa haki na kwamba hawezi tu kufuta deni lako. Lakini kutokana na jinsi anavyojali amenishauri kuuza sehemu ya mali yangu kwa ajili yako. Na hii nimelifanya. Fedha za kulipa deni lako, ninazo na ninakupa kwa furaha. Nenda kwa Baba kesho na umpe fedha hizi na Mungu akubariki.”

Hata hivyo, badala ya kushukuru, Rashid alimwangalia mtoto wa mwenye nyumba kwa dharau na kwa majivuno akamwambia: "Mimi sina lolote nawe, na wala sihitaji msaada wako. Nikishamlipa  Baba yako nitajitunza mwenyewe.
Chukua fedha zako uondoke”. Akamtupia yule mtoto wa mwenye nyumba zile fedha na kumwelekeza mlangoni ili atoke. Mtoto wa mwenye nyumba alikaa kimya. Akimwangalia Rashid kwa masikitiko akaondoka.

Siku ya pili mwenye nyumba akaja mwenyewe. Akiwa na hasira na ya kuchanganyikiwa Rashid angefanya nini kama zi kujitupa chini ya miguu yake kuomba huruma na msamaha? Mwenye nyumba akamjibu: “Jana usiku nilituma huruma na msamaha kwako kupitia mtoto wangu. Hukumkubali yeye wala chochote. Nafasi imepotea; Sina njia nyingine ya kukuhurumia’’. Rashid afanye nini? Mara akatolewa katika nyumba na kutupwa barabarani na nyumba Ikafungwa. Nyumba hadi nyumba, mji hadi mji alipita akiomba mpaka siku moja kutokana na njaa na baridi kali, akafa kifo kibaya mbali na nyumbani, mbali na watu wake na marafiki zake na mbali na wapendwa wake.

Mpendwa, je! Wewe pia sio kama huyu Rachid Sultan? Toka wakati ule ulipofahamu tofauti kati ya jema na ovu, madeni yako yamekuwa mbele za Mungu. Yawezkana mara kwa mara umefanya mambo ambayo Mungu amekataza, na kukataa kufanya mambo ambayo amekuagiza. Nyakati fulani ukaamua kufanya mambo mema badala ya yale mabaya. Ukidhani kwamba kwa kufanya hivyo, Mungu atafuta madeni yako.

Kufikiri hivyo, ni kukosea. Nia yako na maamuzi yako mazuri, toba yako na kazi yako nzuri hata maombi yako na kufunga kwako, vyote hivi haviwezi kulipia dhambi zako za kale. Kutenda mambo mema (sasa au hata baadaye) ni kutimiza tu wajibu wako mbele za Mungu. Je! Ni kwa jinsi gani kufanya jukumu lako sasa, na katika siku zijazo, Iwezekaneje basi kufanya matendo mema sasa au hata baadaye, kuweza kufuta dhambi zako za zamani?

Wala hakuna mtu mwingine yeyote anayewza kuomba kwa ajili ya kufutwa kwa dhambi zako. Wao pia wana madeni ya kumlipa Mungu na kimbilio lao ni Mungu peke yake. Maana kila mmoja atatoa hesabu yake mwenyewe mbele za Mungu wa haki siku ile ya hukumu. Mungu anaona kwamba mwenyewe huna njia ya kulipa madeni yako na anajua vema kuliko yeyote kwamba siku ya hukumu inakaribia. Hii ndiyo maana anakuonea huruma na akaamuakukutumia njia ya kukuokoa. Kama mwenye nyumba alivyomtuma mtoto wake kwa Rashid, ndivyo Mungu alivyomtuma Mwanawe wa kiroho,
Yesu Kristo Masihi, akuletee habari njema hii njema. Huyu Yesu ndiye Mwokozi wa ulimwengu kwa sababu katika yeye, Mungu ametoa ukombozi wa dhambi na mauti kwa wanadamu wote.

Mungu amemtuma Yesu, Neno lake la uzima, ili arejeshe amani na uhusiano kati yako na yeye. Ametoa urithi wake alipoacha mbingu na kuja duniani. Aliishi kwa ajili yako na kufa kwa ajili yako. Kwa kumwaga damu yake ya thamani msalabani alikuletea wewe msamaha kutoka kwa Mungu. Leo anakupa msamaha wake wa ajabu, msamaha uliothibitishwa na kufufuka kwake katika wafu.

*Mpendwa, hakua anayeweza kununua msamaha huu kutoka kwa Mungu. Msamaha ni zawadi ya Mungu, ambayo ni Yeye peke yake anayeweza kutoa.*

*Usiongeze katika hesabu ya dhambi zako mashtaka kwa kukataa msamaha utokao kwa Masihi. Mkubali Masihi kama mwana wa Mungu aliye mtakatifu mwenye upendo aliolipa kwa ajili ya amani yako- kabla ya neema hii ya Mungu na kujiona umechelewa.*

*Yesu alisema: "Njooni kwangu, nyinyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jitieni ni nira yangu, mjifunze kwangu kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu, Kwa maana nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi ", (Mathayo 11: 28-30).*

*Kama unataka ushindi dhidi ya dhambi na kujifunza zaidi juu ya Yesu Masihi, tuko tayari kukutumia vitabu vya kukusaidia zaidi. Tafadhali tuma barua yako kwa anuani moja wapo kulingana na mahali unakoishi.*

---

‘’Ni lazima ulipe deni lako, kwa sababu malipo ya deni lako la baadaye hayataweza kufunika deni lako la nyuma’’

Kukusaidia kuelewa zaidi kuhusu Yesu Masihi, tuko tayari kukutumia vijitabu vingine.

Tafadhali wasiliana nasi kupitia anuani zifuatazo:

**HAMASA YA MILELE**

Box 11795 Arusha, Tanzania

Simu: **0767-288.053**, Barua pepe: **hymilele@gmail.com**

**LIFE CHALLENGE,** Box 50770, Nairobi, Kenya

Simu: **0728-858.333,** Barua pepe: **coast@lifechallenge.de**